**“Mchungaji” Wa Iran**

Nadhani umesikia habari ya “mchungaji” wa Iran aliyepandishwa kizimbani mara tatu wiki hii kule Iran kwa sababu ya kutamka Jina la Yesu Kristo. Habari hii imetekaka ya vyombo fulani vya habari ulimwenguni. Hata katika kanisa la Bwana wapo waliotekwa na habari hii.

Hali hii sio ngeni kwa sasa kwa hapa ulimwenguni. Kwa miaka mia na mamia watu ambao walikuwa “wanamkiri Kristo”, walikuwa wakiuliwa kwa sababu ya ungamo lao. Ndio nimetoka kumaliza kusoma kitabu ambacho kwa kiasi kikubwa kinaelezea mauaji dhidi ya “kanisa changa” yaliyotokea kule Romania na Urusi ya zamani, mnamo muongo wa kuanzia 1950 na 1960. Kitabu kinaelezea habari ya vifo vya watu kadha wa kadha waliodai kuwa wakristo. Kitabu hiki kinaendelea kudai kwamba maelfu kwa maelfu ya watu waliteseka kwa njaa, walipigwa, walibakwa, waliuawa kwa namna mbalimbali, kwa sababu wanaume kwa wanawake walikuwa wanamkiri Kristo mbele ya watawala wa kikomunisti. Hivyo, inasikitishaje hili kutokea leo, na ili hali limekuwa likitokea kwa mamia na mamia ya miaka. Nami ninamsikitikia huyu Mu-irani na familia yake. Yuko katika hali inayosikitisha na ya fedheha.

Sasa swali tulilo nalo ni hili: “endapo huyu “mchungaji” anauawa kwa kumkiri Kristo, Mungu atamhukumia adhabu ya Jehanam?” “Je, Mungu atamhukumia adhabu ya mateso ya milele na milele kwa kutobatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi?”

Kabla hatujaanza, yapo mengi yahusianayo  na suala hili. Pengine alikuwa ni muumini na akaanguka? Labda ni muumini mwaminifu katika kanisa la Bwana na vyombo vya habari vinamwita “mchungaji” kwa sababu hawajui jina jingine la kumwita? Labda ni mchungaji wa madhehebu fulani na ameisikia kweli kupitia World Radio, WBS, au WVBS na ameikataa kweli? Nani ajuaye? Kwa masilahi ya hoja,tuchukulie kuwa alikuwa mchungaji wa dhehebu fulani na kwamba hajawahi kuisikia kweli. Na tuchukulie kuwa ameuawa kwa kumkiri Kristo. Hatima yake ya milele itakuwa wapi?

Kwanza, nataka kushughulikia wazo hili : “Mungu ni Mungu na Mungu aweza kufanya lolote alitakalo. Na kama Mungu anataka kumwokoa mtu huyu, pasipo ubatizo, kwa sababu ya imani yake kubwa, basi Mungu anaweza.

Tunatakiwa kukumbuka kwamba Mungu siyo mwongo, Tito 1:2. Na Mungu alishaainisha taratibu za mtu atakayeokoka, naye hakunena kwa nafsi yake mwenyewe, nasi vivyo. Katika Marko 16:16 Yesu alisema, “aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.” Vilevile Yesu alisema “Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu…usisitaajabu kwa kuwa nilikwambia hamna budi kuzaliwa mara ya pili…Bali yeye aitendaye kweli huja kwenye nuru,” Yohana 3:5,7 21. Paulo alisema, “Katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu , na wao wasioitii injili ya Bwana wetu Yesu,” 2Wathesalonike 1:8. Tunaposhughulikia kisa hiki, tunaongea kwa nafsi zetu wenyewe au kwa nafsi ya Mungu? (Kitabu, Sura, mstari.)

Ndiyo, Mungu ni mtawala na anaweza kumwokoa amtakaye, Warumi 9. Walakini, Mungu ambaye ndani yake hakuna kubadilika wala kivuri cha kugeuka-geuka tayari ameshasema atakayemwokoa, Yakobo 1:17; Hesabu 23:19. Kwa kuwa habadiliki, wala hasemi uongo, basi hitimisho pekee tunaloweza kufikia katika kulitumia kwa hali neno, ni kwamba endapo huunganiki na damu ya mwanakondoo katika ubatizo, huwezi kuokoka!

Natamani kama tungerudi nyuma siku zile ambapo tungesema tu kama Yesu alivyosema, siyo kusema kwa nafsi zetu, bali anachotaka Mungu, Yohana 8:28; 12:49-50. Kwa maana Yesu asingepita aliyosema Baba; Hatutakiwi kupita yaliyoandikwa, 1 Wakorintho 4:6, kulifanya neno la Mungu likaonekana kana kwamba ni kigeugeu

Pili, tunaingiaje mbinguni bila damu ya Yesu? Katika Warumi 3:27,  Paulo anafundisha kwamba tumeokolewa kwa “sheria ya imani.” Katika warumi 5:1 Paulo anafundisha “tuna amani na Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.” Kisha, katika Warumi 6:3, Paulo anatufundisha jambo ambalo sheria ya imani inatuambia tufanye ili tuwe na amani na Mungu. Nalo ni kwa njia ya “kubatizwa katika Kristo.” Katika Ubatizo ndiko tunakokutana na damu ya mwanakondoo, Ufunuo 1:5. Hivyo, kwa kifupi, wale ambao wangeshikilia kwamba Mungu

amwingize mbinguni huyu “mchungaji” kama anataka kufanya hivyo, Mungu atakuwa anampita mwanakondoo wa Mungu, damu ya Kristo. Na kama Yesu anaweza kupitwa, kwa nini alikufa basi? Kwa nini alichinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, ikiwa mauti yake si muhimu kwa mtu kuokolewa!

Tatu, wale wanaotaka “mchungaji” huyu aokolewe kwa mtaji wa kumkiri Yesu tu:

1) “wamemwokoa ” mtu bila damu ya mwanakondoo, Ufunuo. 1:5.
2) “Wamemwokoa” mtu bila kumwingiza katika kanisa, Matendo ya mitume 2:41-47; 1 Wakorintho. 12:13.
3) “Wamemwokoa” mtu bila kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu , Matendo ya Mitume 2:38.
4) “Wamemwokoa” mtu ambaye ni nabii wa uongo, Mathayo 7:21-23.
5) “wamemwokoa ” mtu ambaye hajamsikiliza Yesu wala kumtii, , Luka 6:46.
6) “wamemwokoa” mtu ambaye hajazaliwa mara ya pili , Yohana 3:3-7.
7) “Wamemwokoa” mtu ambaye Yesu hatamkabidhi kwa Baba , 1 Wakorintho. 15:24.
8) “Wamemwokoa” mtu ambaye “hajaposwa…. kwa ajili mume mmoja,” 2 Wakorintho. 11:2.
9) “Wamemwokoa” mtu ambaye amekufa katika dhambi zake, Wakolosai. 2:11-12

Ninapohitimisha karipio hili dogo: tayari najua nitaitwa mshika sheria, au nitapewa kajina kengine kazuri zuri. Na endapo unajisikia kunipa jina, lakini hulioni, naweza kukusaidia. Haina shida. Nitumie barua pepe tu. Lakini ujue hili, sitaacha hisia zangu zinipelekeshe hadi kufikia kuyapita yaliyoandikwa. Maana namtumikia mwokozi mfufuka, ambaye asingeyapita yale aliyosema Baba. Ingawaje hisia zake zilimpelekea hadi machozi, bado hakulifanya neno la Mungu lionekane kigeugeu. Wewe?

Hivyo, namlilia huyu “mchungaji.” Nimeguswa na habari yake. Sipendi nafsi iwayo yote ipotee. Walakini hakuna mtu atakayeingia mbinguni bila “kuoshwa kwa damu ya mwanakondoo” Ufunuo 1:5

Tafadhari zingatia mistari hii, na ukumbuke ya kwamba “maandiko hayatanguki”

1) **Luka 6:46** “Na kwa nini mnaniita, Bwana, Bwana, walakini hamyatendi nisemayo? “
2) **Mathayo 7:21-23** [21] “Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa Mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni [22] Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? [23]Ndipo nitawaambia dhahiri, sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu”
3) **Matendo ya Mitume 2:38** “ Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu .”
4) **Matendo ya Mitume 6:7 “**Neno la Mungu likaenea; na hesabu ya wanafunzi ikazidi sana katika Yerusalemu; jamii kubwa ya makuhani ikaitii ile Imani”
5) **Matendo ya Mitume 9:18** “Mara vikaanguka machoni pake vitu kama magamba, akapata kuona, akasimama, akabatizwa”
6) **Matendo ya Mitume 10:47-48** [47] “Ni nani awezaye kuzuia maji, hawa wasibatizwe, watu waliopokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi? Akaamuru wabatizwe kwa Jina Yesu Kristo, ndipo wakamsihi azidi kukaa siku kadha wa kadha.”
7) **Matendo ya Mitume 5:29** “Petro na mitume wakajibu, wakisema, imetupasa kumtii Mungu kuliko wanandamu.”
8) **1 Wakorintho 12:13** “ Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani; ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru; nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja.”
9) **1 Petro 3:21”** Mfano wa mambo hayo ni ubatizo, unaowaokoa ninnyi pia siku hizi; (siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu), kwa kufufuka kwake Yesu Kristo”